Watu wa aina saba atawapa kivuli Mwenyezi Mungu Mtukufu siku ambayo hapatokuwa na kivuli isipokuwa kivuli chake

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Watu wa aina saba atawapa kivuli Mwenyezi Mungu Mtukufu siku ambayo hapatokuwa na kivuli isipokuwa kivuli chake: Kiongozi muadilifu, na kijana aliyekulia katika ibada ya Mwenyezi Mungu, na mtu ambaye moyo wake umetundikwa katika misikiti, na watu wawili walipoendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wakakutana kwa ajili yake na wakaachana kwa ajili yake, na mwanaume aliyeitwa na mwanamke mwenye wadhifa na uzuri, akasema: Hakika mimi ninamhofu Allah, na mtu aliyetoa sadaka akaificha mpaka usijue kushoto kwake unachotoa kulia kwake, na mtu aliyemkumbuka Mwenyezi Mungu akiwa faragha, yakabubujika machozi macho yake".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake]

Alitoa habari njema Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya aina saba za waumini atakaowapa kivuli Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kivuli cha Arshi yake siku ambayo hakutokuwa na kivuli isipokuwa kivuli chake: Wa kwanza: Imamu muadilifu katika nafsi yake na si muovu, na ni muadilifu kwa raia wake na si dhalimu; naye ni yule mwenye mamlaka ya juu, na anaungana naye kila kiongozi atakayeongoza chochote katika mambo ya waislamu akafanya uadilifu ndani yake. Wa pili: Ni kijana aliyekulia katika ibada ya Mwenyezi Mungu, na akaumaliza ujana wake na uchangamfu wake, mpaka akafishwa katika hali hiyo. Wa tatu: Ni mtu ambaye moyo wake umetundikwa katika msikiti, pindi akitoka mpaka hatulizani mpaka arudi ndani yake kwa sababu ya mapenzi makubwa na wingi wa kushikamana na msikiti na kuendelea kubaki ndani yake kwa moyo, hata kukitokea dharura akiwa msikitini akatoka nje ya msikiti. Wa nne: Ni watu wawili kila mmoja alimpenda mwenzake kweli kweli kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na wakadumu katika mapenzi ya dini na ikawa haikuwakatisha sababu yoyote ya kidunia zaidi kukutana kweli au la sivyo mpaka kifo kikawatenganisha. Wa tano: Na mwanaume aliyetakwa na mwanamke ili kumtumia kufanya machafu, naye ni mwanamke mwenye msingi mzuri na heshima na ukoo mtukufu na cheo na mali na uzuri, akakataa na akasema kumwambia: Hakika mimi ninamuhofu Allah. Wa sita: Ni mtu aliyetoa sadaka ndogo au nyingi, na hakutaka kuonekana ndani yake, bali aliificha mpaka haukujua mkono wa koshoto kwake kilichotolewa na mkono kulia kwake. Wa saba: Ni mtu aliyemtaja Mwenyezi Mungu kwa moyo wake kwa kumkumbuka, au kwa ulimi wake kwa kufanya dhikri, akiwa faragha mbali na watu, yakabubujika machozi kutoka machoni mwake kwa hofu na kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu Mtukufu.